Toleo la 23

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Juni 30, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

# TAHARIRI

## HONGERA SERIKALI KWA KUUENZI UTAMADUNI



Mhariri
**JOHN MAPEPELE**

Tanzania inakwenda kuandika historia ya kuandaa tamasha la kwanza la kihistoria la kitaifa la Utamaduni Julai 1-7, 2022 jijini Dar es Salaam.

Tamasha hili linaambatana na shughuli kadhaa ikiwa ni pamoja na maonesho mbalimbali ya vyakula na ngoma za asili, matembezi ya kiutamaduni ( Utamaduni Carnival) na maadhimisho ya siku ya kiswahili duniani.

Maadhimisho haya yamelenga kuenzi na kuitangaza Tanzania duniani kupitia Utamaduni ikiwa ni pamoja na lugha aushi ya kiswahili ambayo imetambuliwa UNESCO na kupewa siku maalum ya kuadhimishwa ambayo ni Julai 7 ya kila mwaka.

ınapenda kuazima maneno ı Mhe. Rais Samia Suluhu assan aliyoyatoa hivi karibuni akati akilipokea kombe la ınia la FIFA kuwa viongozi wa izara wamekuwa wabunifu a kutumia sekta za michezo, ınaa na Utamaduni kuleta raha kwa watanzania na kuitangaza Tanzania.

Nasi tunaungana na Mhe. Rais Samia kuupongeza uongozi madhubuti wa Wizara chini ya Waziri Mohamed Mchengerwa kwa kuendelea kuwa wabunifu.

Ni matarajio yetu kuwa wananchi kutoka sehemu mbalimbali watashiriki kikamilifu kuja kujifunza na kujionea hazina ya tamaduni mbalimbali za nchi yetu.

Pia wananchi watapata fursa kushiriki kwenye usiku wa taarabu na kongamano la kiswahili na kujifunza namna kiswahili kilivyotumia katika ukombozi wa bara la Afrika kutoka kwenye shuhuda za viongozi wa nchi mbalimbali za Afrika ambao watakuwepo.

**BODI YA WAHARIRI**

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Dkt. Hassan Abbasi**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Saidi Yakubu**

Mhariri
**John Mapepele**

Waandishi
**Eleuteri Mangi**
**Shamimu Nyaki**

Wapiga Picha
**Joseph Kigingi**
**Projestus Binamungu**

Msanifu
**Abubakar W Kafumba**




# Mhe. Majaliwa Kuhutubia Utamaduni Carnival

Na John Mapepele, **WUSM**, **Dar es Salaam**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa anatarajiwa kuhutubia wananchi kwenye Maadhimisho ya Tamasha la kwanza la kihistoria la Utamaduni kitaifa Julai 2, 2022 Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam mara baada ya matembezi ya kiutamaduni.

Tamasha hilo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliyoyatoa kwenye Tamasha la Utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro la kutaka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuandaa tamasha kubwa la kitaifa la utamaduni litakaloshirikisha mikoa yote ya Tanzania ili kutangaza hazina ya utamaduni wa makabila ya Tanzania Duniani.

Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa, amefafanua kuwa tamasha hilo litaambatana na matembezi maalum ya kitamaduni (Utamaduni Carnival) katika jiji la Dar es Salaam ambayo yameandaliwa njia maalum za kupita ikiwemo daraja la juu la Mfugale, Kijazi, Tanzanite na daraja la mwalimu Nyerere.

Amesema, tamasha hilo litatoa fursa kwa makabila yote nchini kuonesha tamaduni zao kupitia ngoma na vyakula vya asili ili kukuza utalii wa kiutamaduni.

Aidha, amewataka watanzania kujitokeza kushiriki kwenye tamasha hilo la kwanza la kitaifa ambalo licha ya kutoa burudani, litaonesha vitu muhimu vya kiutamaduni na kutoa fursa kwa wageni kujifunza.

Ameongeza kuwa, tamasha hilo litakuwa la siku tatu ambapo siku inayofuata ya Julai 3, 2022 itakuwa na tukio maalum la mirindimo ya taarabu ambapo limeainishwa kama usiku wa taarabu utakaofanyika eneo la ufukwe wa Coco Beach maarufu kwa wachoma mihogo kuanzia saa 8:00 hadi saa 6:00 usiku.

Amesema shamrashamra hizo zitashamirishwa na vikundi mbalimbali vya wasanii kutoka ndani na nje ya Tanzania kama Comoro, Burundi na Kenya, pia wasanii wa taarabu nchini akiwemo Mzee Yusufu, Hadija Kopa, Patricia Hillay, Abuduli Misambano na Aisha Mashauzi watakuwepo kutumbuiza usiku huo.



# Naibu Spika Mhe, Zungu Mgeni Rasmi Usiku wa Taarabu

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mussa Azan Zungu anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Usiku wa Taarabu Julai 03, 2022 utakaofanyika katika Fukwe za Coco (CoCo Beach) Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari leo Juni 29, 2022, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla amesema usiku utahusisha muziki wa taarabu asilia na taarabu ya kisasa kutoka ndani na nje ya nchi

"usiku huu utapambwa na mbalimbali akiwemo Mzee Yusuph, Hadija Kopa, Patricia Hillary, Isha Mashauzi, Sabaha Mchacho, Abdul Misambano na wengine wengi" alisema Mhe. Makalla.

Ameongeza kuwa, vikundi mbalimbali ikiwemo First Class , Wana Nakshi Nakshi, Rahat Zaman, Nadi Ikhwan Safaa, Chama Cha Wasanii wa Muziki Zanzibar pamoja na Vikundi vya taarabu kutoka nchini Burundi, Kenya, na. Visiwa vya Comoro vitashiriki

Usiku huo wa taarabu ni muendelezo wa Tamasha la Utamaduni la Kwanza Kitaifa ambalo litafanyika katika Uwanja wa Uhuru Julai 01 hadi 03, 2022 ikiwa ni kuelekea kilelele cha maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani Julai 07, 2022.




# Waziri Mchengerwa: Tuzo za BET ni Nguzo Kuboresha Sanaa Tanzania

Na Mwandishi Wetu, LA, **Marekani**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa, amesema watazitumia tuzo za BET za mwaka 2022 kuona maeneo ya kuboresha zaidi katika usimamizi wa sekta ya sanaa nchini Tanzania.

Waziri Mchengerwa ameyasema hayo baada ya kushuhudia Tuzo za BET za mwaka huu 2022 mjini Los Angeles, California, usiku wa kuamkia leo.

"Tumeshuhudia tuzo hizi ikiwa pia ni maandalizi ya sisi kuandaa tuzo kubwa kwa upande wa Afrika za MTV, ambapo sehemu ya waandaaji wake ni hawa hawa wa tuzo za BET na kuna maeneo ya kisera na kimageuzi tutaendelea nayo baada ya hapo," alisema Waziri Mchengerwa.

Awali, Waziri Mchengerwa alikutana na Makamu wa Rais wa Paramount Africa inayosimamia vituo vya burudani vya MTV na shindano la tuzo za MAMA, Bw. Monde Twala na kukubaliana kukamilisha michakato mbalimbali za kuipa Tanzania nafasi ya kuwa mwenyeji wa tuzo za MAMA kwa mwaka 2023 na kukubaliana pia uwezekano wa kuileta BET Tanzania huko mbele na kushirikiana zaidi katika sekta za sanaa kwa ujumla.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara hiyo aliyeambatana na Mhe Waziri katika tuzo hizo, Dkt. Hassan Abbasi amesema tuzo za BET pia zitaisaidia Tanzania kuboresha tuzo zake za ndani na usimamizi wake kwani nazo zinaweza kuwa kubwa kama za BET.




# Kuelekea Tamasha la Kitaifa la Utamaduni, Mhe. Mchengerwa awapigia pande wasanii

**Na John Mapepele, WUSM, Dar es Salaam**

Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo. Mhe, Mohamed Mchengerwa amewataka wasanii kuchangamkia fursa za Sanaa katika mashindano ya dunia ya mpira wa miguu nchini Qatar.

Amesema, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuwapigania wasanii kupata fursa mbalimbali za ajira za sanaa, imewatafutia fursa husika wasanii katika fani mbalimbali.

"Wizara inatoa wito kwa wasanii mbalimbali nchini kufuatilia Link hii chini https://www.qatar2022.qa-/en/opporrtunities/community-engagement/register-as-artist ili kuchangamkia fursa husika" amesisitiza Mhe. Mchengerwa

Amesema Wizara itakuwa tayari kusaidia pale penye uhitaji ili kufanikisha zoezi husika.



# Wasanii Tanzania Kufunguliwa Milango Zaidi Soko la Hollywood

**Na Mwandishi Wetu, LA, California**

Wasanii mbalimbali wa Tanzania hasa wa muziki na filamu wameahidiwa kufunguliwa milango zaidi katika soko na kiwanda kikubwa zaidi duniani cha burudani cha Hollywood nchini Marekani ili kupata mafanikio zaidi katika kazi zao.

Ahadi hiyo imetolewa na mmoja wa watendaji na wawekezaji wa masuala ya sanaa na burudani nchini Marekani, Bw. Tyrone Davis, alipokutana na kufanya mazungumzo ya kina na Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka nchini Tanzania, Dkt. Hassan Abbasi, siku ya Jumanne Juni 28, 2022, jijini hapa.

Pamoja na sasa kujikita zaidi katika kampuni za fedha na masuala ya teknolojia nchini Marekani akiwa Mtendaji Mkuu wa taasisi ya Urban Icon na pia Mwenyekiti wa taasisi ya kifedha ya IN CARD, Bw. Davis anabaki kuwa mmoja wa wadau wakubwa wa Hollywood.

Katika miaka yake ya takribani miaka 20 katika kiwanda cha Burudani nchini Marekani, Bw. Davis anaendelea kubaki mmoja wa watu wanaofahamiana na kila mdau muhimu wa Hollywood akiwa amefanya kazi na wasanii nguli wa zamani kuanzia MC Hammer, Lionel Richie na produza mwenye tuzo 38 za Grammy, Bw. Quincy Jones, miongoni mwa wasanii wengine wengi.

"Wasanii wa muziki wa Tanzania wanavipaji hivyo wanapaswa kutafutiwa namna ya kuingia zaidi katika soko kubwa kama la Hollywood kuanzia fursa za kurekodi na wasanii wakubwa, kusainiwa na rekodi kubwa ili waendelezwe na kukua zaidi hadi kushirikishwa katika matamasha makubwa.

"Kwa wale wa filamu ni muhimu nao washiriki filamu kubwa na sisi diaspora tulioko huku turudi katika nchi kama Tanzania na kuwekeza miundombinu ya kisasa ya sanaa kama studio. Kupitia kampuni na mitandao yangu tutafungua njia hiyo kwa kuratibu pamoja programu ya kimkakati pamoja na Serikali ya Tanzania," aliahidi Bw. Davis.



# Dar es Salaam ipo tayari kwa Tamasha la Kwanza la Kitaifa la Kiutamaduni

Na Eleutri Mangi - **WUSM, Dar es Salaam**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Saidi Yakubu pamoja na wataalamu wa mkoa ra Dar es salaam wakiongozwa na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo Bw. Lawrence Malangwa wamekagua njia itakayotumika wakati wa matembezi ya kiutamaduni ambayo yatafanyika Julai 2, 2022 jijini Dar es Salaam.

Maeneo yatakayopita matembezi hayo kwa magari ambayo yatakuwa na vikundi mbalimbali vya ngoma kutoka mikoa yote nchini yataanzia Uwanja wa Uhuru kuelekea daraja la Mfugale, daraja la Kijazi Ubungo, Morocco, Namanga, Coco Beach, daraja jipya la Tanzanite, Posta, Kariakoo, Stesheni, Mtoni kwa Azizi Ally, Temeke, Mwembeyanga na kurudi Uwanja wa Uhuru.

Matembezi hayo yatakuwa ya aina yake ambayo kila mkoa utakuwa kwenye gari lake la wazi na kuonesha tamaduni zao. Wakazi wa jiji la Dar es Salaam wamepata fursa adhimu ya kuwa wenyeji wa Tamasha la Utamaduni la Kwanza Kitaifa ambapo kwa mujibu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo litafanyika kila mwaka kwa mzunguko kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine.



# Rais Samia Mgeni Rasmi Siku ya Kiswahili Duniani

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa Mgeni Rasmi katika Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yatakayofanyika kitaifa Julai 07, 2022 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari leo Juni 29, 2022 , Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla, amesema kuwa, analishukuru Shirika la UNESCO nchini kwa kuendelea kuipa heshima lugha ya Kiswahili kwa kuadhimisha siku hiyo maalumu kila Julai 7.

"maadhimisho haya kwa mwaka huu ni ya kipekee sana , tunatarajia kupata wageni wengi mashuhuri kutoka ndani na nje ya nchi, akiwemo Rais Mstaafu wa Msumbiji Mhe.Joachim Chisano, Rais Mstaafu wa Namibia Mhe. Sam Nujoma, hii ni heshima kubwa kwa mkoa wetu " alisema Mhe. Makalla.

Ameongeza kwa kueleza kuwa, maadhimsho hayo yatahusisha shughuri mbalimbali ikiwemo kongamano kuhusu mchango wa lugha ya Kiswahili katika Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika, litakalofanyika Julai 06, 2022 ambapo Balozi Mstaafu Mhe. Ame Mpungwe ataongoza mada mbalimbali.

Maadhimisho hayo yatatanguliwa na Tamasha la Utamaduni la Kwanza Kitaifa ambalo litafanyika katika Uwanja wa Uhuru kuanzia Julai 01 hadi 03, 2022.



# Mhe. Makalla Apongeza Ubunifu wa Tamasha la Utamaduni

Na Eleuteri Mangi - **WUSM, Dar es Salaam**


Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla ameipongeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ubunifu wa kuja la Utamaduni la Kwanza Kitaifa kwa lengo la kutoa fursa kwa kila mkoa kuonesha utamaduni wake.

Mhe. Makalla amesema hayo Juni 29, 2022 wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es salaam ambapo aliwakaribisha wageni wote wanakuja kwenye tamasha hilo mkoni humo na amewahakikishia ulinzi na usalama wakati wote wa tamasha.

"Watu wa Dar es Salaam tusijifungie ndani, mjitokeze kwa wingi nendeni Uwanja wa Uhuru, kama unataka kujua chakula cha Kihaya matoke haya, kama unataka kujua utamaduni wa Lindi, utamaduni wa Singida, Morogoro, wa Kilimanjaro, utamaduni wa Pwani, mtaona pale Uwanja wa Uhuru kuanzia Julai 1-3, 2022" amesema Mkuu huyo mkoa.

Aidha, Mhe. Makalla amesema tamasha hilo litapambwa kwa matembezi ya Utamaduni yakayofanyika Julai 2, 2022 yatapita maeneo ya vivutio vya jiji hilo ikiwemo madaraja yenye mvuto wa aina yake daraja la Daraja la Julius Nyerere, daraja jipya la Tanzanite, daraja la Kijazi Ubungo na daraja la Mfungale.

Matembezi ya kiutamaduni, yanafanyika katika nchi za Brazil, Uingereza, Cuba na sasa Tanzania kwa namna ya pekee mkoa wa Dar es Salaam.



# WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU**


## Mawasiliano

P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz